MCHANGO, MAENDELEO NA CHANGAMOTO ZINAZOKABILI TAALUMA ZA TAFSIRI NA UKALIMANI KATIKA KISWAHILI

Pendo S. Malangwa
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania

Utangulizi

Tafsiri na ukalimani ni miongoni mwa dhana maarufu sana masikioni mwa wasomi na wasio wasomi. Hata hivyo, taaluma hizi huchanganywa sana zinapotajwa katika maeneo mbalimbali zinamotumika. Tafsiri na ukalimani ni pacha wanaochanganya watu wengi, hasa wale ambao hawajazama katika kujifunza tofauti zilizopo baina ya taaluma hizi. Wengi hudhani kwamba dhana hizi ni kama kitu kile kile. Mambo ambayo huwafanya watu wazichanganye taaluma hizi licha ya ukweli kwamba taaluma hizi zinatofautiana ni kama ifuatavyo:

i. Zote zinahusisha zoezi la uhawilishaji wa mawazo au ujumbe kati ya lugha mbili, yaani lugha chanzi na lugha lengwa.
ii. Zote zinahitaji mfasiri awe na umahiri katika lugha mbili, moja ikiwa ni lugha mama au lugha anayoifahamu kwa viwango vya lugha mama na nyingine ikiwa ni lugha ya pili ambayo amejifunza na kuijua vizuri.
iii. Zote zinatumika kama kiungo baina ya watu wanaozungumza lugha tofauti ambao wana haja ya kuwasiliana.
iv. Zote zinaweza kutumika kama nyenzo za kukuza lugha na utamaduni kupitia uongezaji wa msamiati mpya unaoundwa katika mchakato wa uhawilishaji, matumizi ya lugha katika maandishi (hasa kwa lugha ambazo hazijaandikiwa sana), kukuza fasihi kwa kuiingizia mitindo ya uandishi kutoka utamaduni wa matini chanzi.
v. Zote zinahitaji mtendaji awe na zana za kufanyia kazi. Mfano wa zana za kufanyia kazi katika tafsiri na ukalimani ni pamoja na kamusi, ensaiklopidia na marejeleo mengine katika lugha chanzi na lengwa yanayozungumzia mada ya matini husika.
vi. Zote zinazingatia utamaduni wa lugha chanzi na lugha lengwa. Kwamba mkalimani na mfasiri wanapaswa kufahamu na kuzingatia utamaduni wa jamii za lugha chanzi na lugha lengwa.

Kutokana na mkanganyiko uliopo, ni vyema tukaanza mjadala wetu kwa kuziangalia dhana hizi mbili kwa undani. Ukalimani, kama anavyofafanua Pöcchak (2004), ni taaluma inayohusu uhawilishaji wa mawazo au ujumbe ulio katika mazungumzo kutoka lugha moja (lugha chanzi, LC) kwenda lugha nyingine (lugha lengwa, LL). Kwa upande mwingine, tafsiri ni zoezi la uhawilishaji wa mawazo yaliyo katika maandishi kutoka lugha chanzi kwenda katika lugha lengwa (Mwansoko na wenzake, 2006). Katika fasili hizi ni dhahiri kwamba ukalimani unahusu uhawilishaji wa matini iliyo katika muundo wa mazungumzo ilhali tafsiri inahusu uhawilishaji wa matini iliyo katika maandishi. Yapo mambo mengi ya kiutendaji na kinadharia yanayoshadidia kwamba ukalimani na tafsiri ni taaluma mbili tofauti, ikiwa ni pamoja na historia ya taaluma hizi, zana za kufanyia kazi, mchakato wake na utumizi wa marejeleo, aina na ujuzi wa hadhira, na kadhalika.

Shughuli za tafsiri na ukalimani hufanyika kila siku katika maisha ya mwanadamu (Malangwa, 2012). Kwa mfano, katika ukanda wa Afrika Mashariki, si jambo la ajabu kukuta ukalimani ukifanyika kati ya Kiswahili na lugha za wenyeji (lugha za jamii), hasa katika mahakama na

nyumba za ibada. Aidha, katika historia yake, maandishi mengi ya awali katika lugha ya Kiswahili na lugha za wenyeji yalitokana na juhudi za kutafsiri. Halikadhalika, wageni kama vile wamisionari waliweza kuwasiliana na wenyeji wa ukanda huu katika kutekeleza majukumu mbalimbali ya kueneza dini kwa njia ya ukalimani. Aidha, katika ufundishaji wa Kiswahili, maarifa mengi ya kiisimu na kifasihi yamehawilishwa kutoka maandishi ambayo ama yalikuwa katika lugha ya Kiingereza au katika Kiswahili, na kwa baadhi kutoka katika Kifaransa au Kijerumani, kutegemeana na wakoloni waliotawala. Kwa ujumla, umuhimu wa taaluma hizi hauelezeki na ndio maana juhudi mbalimbali zinafanyika ili kuziendeleza taaluma hizi. Makala haya yanapambanua jinsi taaluma hizi zinavyosaidia katika kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili, kama lugha na kama taaluma. Aidha, makala yanaangalia pia maendeleo yaliyofikiwa katika taaluma hizi na changamato zilizopo.

Mkabala na Mbinu

Mkabala uliotumika katika utafiti na uandishi wa makala haya ni mkabala wa kimaelezo ambao haukuhusisha data ya kitakwimu kwa kiasi kikubwa. Data ya utafiti huu imekusanywa kwa kutumia mbinu ya upitiaji wa machapisho na usaili. Upitiaji wa machapisho mbalimbali kutoka mtandaoni na katika maktaba za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ulifanyika ili kufanikisha malengo ya makala haya. Usaili pia ulifanyika kwa sampuli ya walimu wa vyuo vikuu wapatao 12 walioteuliwa kwa mbinu ya malengo maalum kutoka katika vyuo vikuu 12 nchini Tanzania. Watafitiwa walioshirikishwa katika utafiti huu ni walimu wa masomo ya lugha (Kiswahili na Kiingereza) wanaofundisha katika vyuo hivi. Kupitia usaili, data ya idara, kozi zinazofundishwa na idadi ya walimu wanaofundisha tafsiri na/au ukalimani ilipatikana. Usaili pia ulikusudiwa kubaini maendeleo mengine yaliyofikiwa katika taaluma za tafsiri na ukalimani pamoja na changamoto zinazojitokeza. Aidha, kupitia utafiti huu mapendekezo mbalimbali yalitolewa kama itakavyoelezwa katika sehemu ya 5 ya makala haya.

Mchango na Maendeleo ya Tafsiri na Ukalimani

Kimachapisho

Katika taaluma ya tafsiri na ukalimani tunapozungumzia machapisho moja kwa moja tunarejelea tafsiri kwani ukalimani unahusu masuala ya uzungumzaji na tafsiri inahusika na lugha ya maandishi. Kumbukumbu zinaonesha kwamba tafsiri katika Kiswahili ilianza katika karne ya 16 na tafsiri ya kwanza ilikuwa ni utenzi wa Kiarabu ujulikanao kama *Hamziyya*. Utenzi huu ulitafsiriwa katika Kiswahili na Bwana Aidarus bin Athuman aliyeishi Kaskazini mwa Kenya miaka ya 1700-1950 BK (Mwansoko na wenzake, 2006). Baada ya uhuru, vitabu vingi vya fasihi vilifasiriwa katika Kiswahili na watangulizi wetu, mfano J. K. Nyerere[1] na wanamapinduzi wengine wa Afrika Mashariki.

Wataalamu wa Kiswahili wamekuwa wakitumia mbinu ya tafsiri katika kuandika na kuchapisha vitabu mbalimbali, hali ambayo imewasaidia kujipatia umaarufu, kupanda vyeo vya kitaaluma, kuandaa vitabu vya Kiswahili katika taaluma mbalimbali za Kiswahili, na kadhalika.

Aidha, kumekuwa na machapisho kadhaa yanayozihusu taaluma hizi katika Kiswahili. Ukiachilia mbali kitabu maarufu cha *Kitangulizi cha Tafsiri* (Mwansoko na wenzake, 2006), kuna machapisho mengine ya taaluma hizi katika Kiswahili, ikiwa ni pamoja na *Tafsiri na*

[1] Aliyetafsiri kazi za fasihi za mwandishi maarufu wa fasihi ya Kiingereza, Shakespeare.

Kufasiri (2010) cha Hamadi Mshindo na *Tafsiri na Ukalimani* (2012) cha Simiyu Wanjala. Wataalam wa eneo hili wamekuwa wakichapisha makala katika majarida mbalimbali ili kusukuma mbele maendeleo ya taaluma hizi katika Kiswahili.

Kimsamiati

Kupitia shughuli za ukalimani na tafsiri zinazofanyika kila uchao, kuna msamiati mwingi sana unaoundwa kwa kujua au kutokujua. Hii hasa hutokea pale ambapo wafasiri au wakalimani wanapokutana na maneno ambayo hayana visawe katika Kiswahili. Wengi wao huunda maneno ambayo yanawasaidia katika kuwasilisha ujumbe unaotakiwa. Maneno yanayoundwa na wakalimani au wafasiri katika vyombo vya habari huvuma na kuenea kwa wakati mfupi miongoni mwa wazungumzaji wa Kiswahili. Msamiati kama *kiyoyozi*, *king'amuzi*, *runinga*, na kadhalika umetokana na juhudi za watu kutafsiri masuala ya kiuvumbuzi katika Kiswahili. Hii inachangia sana katika kukuza msamiati wa Kiswahili na kukifanya Kiswahili kiweze kutumika katika maeneo mapana zaidi.

Kwa upande mwingine, tangu taaluma hizi zianze kufundishwa kwa Kiswahili juhudi kubwa imefanyika kutafsiri istilahi za tafsiri na ukalimani pamoja na maarifa yake kutoka Kiingereza kwenda katika Kiswahili. Kwa kufanya hivi, msamiati mwingi sana umeundwa na kuongezeka katika taaluma za Kiswahili. Hii imewasaidia sana wataalamu na wanafunzi katika kufundisha na kujifunza kwa urahisi na hata kuandika makala katika Kiswahili.

Katika Ufundishaji

Taaluma za Kiswahili zimefanikiwa kupanua mawanda yake kinadharia na kivitendo kwa kuhawilisha dhana au nadharia za kiisimu na kifasihi kutoka katika lugha nyingine ambazo tayari zimeandikiwa kuhusu suala hilo. Si ajabu kumkuta mhadhiri wa Kiswahili akiwatangazia wanafunzi wasome vitabu vilivyoandikwa kwa Kiingereza, kama vile vitabu vya isimu na fasihi vilivyoandikwa na wataalamu kama vile Chomsky, Finnegan na Katamba, kwa kutaja wachache ili kujipatia maarifa fulani. Maarifa wanayoyapata katika vitabu hivyo huyawasilisha kwa njia ya tafsiri. Kwa ujumla, ni jambo lisilo na ubishi kwamba ufundishaji wa taaluma za Kiswahili katika elimu ya juu umekitwa katika kutafsiri maarifa na baadaye kutumia tu data ya Kiswahili kufafanua dhana zinazohusika. Hii imekuwa ni nyenzo muhimu sana katika ufundishaji na ujifunzaji taaluma za Kiswahili.

Aidha, kumekuwa na juhudi za kimakusudi katika idara za Kiswahili na Idara za lugha nyingine kufundisha taaluma za tafsiri na ukalimani kati ya lugha ya Kiswahili na lugha nyingine. Wanafunzi wanaochagua kusoma taaluma hizi si wanafunzi wa lugha pekee. Wanafunzi wa shahada ya ualimu katika masomo mengine kama vile Jiografia na Historia huchagua kusoma tafsiri na (au) ukalimani. Hii imekuwa na mchango mkubwa, hasa kwa wale wanaosomea shahada za ualimu, kwani inawasaidia kuwapatia ujuzi na kuutumia kama mbinu ya kufundishia na wengine kujiajiri. Katika hali halisi, machapisho mengi ya taaluma mbalimbali yameandikwa kwa Kiingereza. Walimu wanaofundisha katika ngazi ya shule ya msingi nchini Tanzania, kwa mfano, hulazimika kufundisha masomo mbalimbali kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Wengi hutumia maarifa ya tafsiri na ukalimani katika kufundisha maarifa mbalimbali yaliyoandikwa katika lugha nyingine, kama vile Kiingereza.

Vyuo Vinavyofundisha Taaluma ya Tafsiri na Ukalimani Tanzania

Tafsiri na ukalimani hufundishwa katika vyuo kadhaa vya Afrika Mashariki, hususan Kenya na Tanzania. Nchini Tanzania, kwa mfano, zaidi ya vyuo vikuu 12 kati ya vyuo zaidi ya 25 hufundisha kozi ya tafsiri na (au) ukalimani. Katika jedwali lililopo hapa chini kuna mifano ya vyuo vikuu vinavyofundisha tafsiri na (au) ukalimani pamoja na idara zake.

Jedwali 1: Mifano ya Vyuo Vikuu na Idara Zinazofundisha Tafsiri na (au) Ukalimani nchini Tanzania

N/M	CHUO KIKUU	IDARA INAYOHUSIKA	KOZI INAYOFUNDISHWA
1	Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM)	Lugha ya Kiswahili na Isimu na Idara ya Lugha za Kigeni na Isimu	Tafsiri
2	Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM)	Kiswahili na Idara ya Lugha za Kigeni na Fasihi	Tafsiri na Ukalimani
3	Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE)	Idara ya Lugha na Isimu	Tafsiri
4	Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE)	Idara ya Lugha na Isimu	Tafsiri
5	Chuo Kikuu cha Mt. Augustino (SAUT) Mtwara (Stella Maris)	Idara ya Kiswahili	Tafsiri na Ukalimani
6	Chuo Kikuu Kishiriki cha Mt. John (St. John)	Idara ya Kiswahili na Idara ya Lugha za Kigeni na Fasihi	Tafsiri na Ukalimani
7	Chuo Kikuu cha Mt. Augustino Tanzania (SAUT)-Mwanza	Idara ya Kiswahili	Tafsiri na Ukalimani
8	Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro (MUM)	Kiswahili na Kiingereza	Tafsiri na Ukalimani
9	Chuo Kikuu cha Tumaini Tanzania na Matawi yake	Idara ya Lugha	Tafsiri
10	Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji (TEKU)	Idara ya Lugha na Isimu	Tafsiri na Ukalimani
11	Chuo Kikuu cha Eckenforde Tanga (Eckenforde)	Idara ya Kiswahili	Tafsiri
11	Chuo Kikuu cha Arusha (Arusha)	Idara ya Kiingereza	Tafsiri
12	Chuo Kikuu Kishiriki cha Jordan Morogoro (Jordan)	Idara ya Kiswahili	Tafsiri na Ukalimani

Chanzo cha data : Malangwa (2012 & 2013)

Data hii inaonesha maendeleo au mafanikio yaliyofikiwa katika taaluma ya tafsiri na ukalimani. Vyuo vikuu vingi vinafundisha kozi ya tafsiri na ukalimani isipokuwa vyuo vichache sana

ambavyo vinafundisha tafsiri tu. Utafiti huu pia unaonesha kwamba katika baadhi ya vyuo, kama vile Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dodoma na Tumaini, kozi ya tafsiri na/au ukalimani hufundishwa mpaka kiwango cha umahiri, na hata Uzamifu.

Aidha, katika utafiti huu imebainika kwamba ni chuo Kikuu kimoja tu kinatoa shahada ya ukalimani na tafsiri (*B.A. Language Studies and Interpretation*), ambacho ni Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro (MUM) wakati vyuo vingine vyote vinafundisha kozi hizi kama sehemu ya kozi za lugha na isimu. Imebainika pia kupitia utafiti huu kwamba katika Chuo Kikuu cha Waisilamu Morogoro kuna maabara na madarasa maalum kwa ajili ya mazoezi ya ukalimani. Wanafunzi wa ukalimani hufanya mazoezi ya kutumia zana mbalimbali za ukalimani (kama vile visikizio, vipaza sauti, paneli, kibanda cha ukalimani, na kadhalika).

Walimu Wanaofundisha Tafsiri na Ukalimani

Ufundishaji wa tafsiri na ukalimani katika vyuo vingi nchini Tanzania hufanywa na ama walimu wa lugha ambao wamesoma tu kozi ya tafsiri au walimu waliosoma kozi ya tafsiri au ukalimani na kuandika tasnifu zao za kuanzia umahiri katika nyanja hizi. Kwa maneno mengine, walimu wanaofundisha tafsiri na ukalimani wamezisoma taaluma hizi katika viwango tofauti vya elimu. Jedwali lililopo hapa chini linaonesha idadi ya walimu katika kila chuo na viwango vyao vya elimu.

Jedwali 2 : Idadi ya Walimu na Viwango vyao vya Elimu katika kila chuo

N/M	**Chuo**	**Idadi ya Walimu**	**Viwango vya Elimu**		
			Shahada ya 1	**Umahiri**	**Uzamivu**
1	UDSM	2		1	1
2	UDOM	1		1	
3	DUCE	*1			1
4	MUCE	1		1	
5	Stella Maris	1		1	
6	St. John	1		1	
7	SAUT-Mwanza	1		1	
8	MUM	*2		2	
9	Tumaini	1		1	
10	TEKU	1		1	
11	Eckenforde	1		1	1
12	Arusha	1		1	
13	Jordan	1		1	

Chanzo cha data : Malangwa (2012 & 2013)

***** Walimu wanaofundisha kwa mkataba maalum wa muda (yaani, part-time)

Data hii inaonesha kwamba angalau katika kila chuo kuna mwalimu anayefundisha tafsiri na/au ukalimani. Hata hivyo, nchini Tanzania ni walimu wachache sana waliosoma tafsiri mpaka kiwango cha uzamivu. Utafiti huu pia umeonesha kwamba baadhi ya walimu wanaofundisha tafsiri na ukalimani hawakusoma kabisa ukalimani katika shahada zao isipokuwa wanatumia uzoefu na ujuzi wao katika taaluma ya tafsiri. Walimu hawa hulazimika kusoma machapisho mbalimbali, kuwasiliana na walimu wengine au kuhudhuria mafunzo na semina za muda mfupi.

Taasisi kama vile Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) huandaa warsha na semina za mafunzo ya ukalimani. Semina hizi huwashirikisha walimu mbalimbali kutoka idara za lugha na fasihi.

Tafsiri na Ukalimani: Nyenzo ya Kufundisha Kiswahili kwa Wageni

Taaluma za tafsiri na ukalimani zimekuwa ni nyenzo kuu za ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni. Walimu wengi wanaofundisha Kiswahili kwa wageni hufundisha kwa njia ya kutafsiri Kiswahili katika lugha za wageni hao. Kwa maneno mengine, tafsiri na ukalimani hutumika kama mbinu za kufundishia Kiswahili kwa wageni kutoka mataifa mbalimbali wanaojifunza Kiswahili. Kwa mfano, Taasisi kama vile TATAKI hupokea wageni wanaokuja kujifunza Kiswahili kutoka nchi kama vile Urusi, Italia, China na Korea. Wengi wao huhitaji kufundishwa kwa mbinu ya tafsiri au ukalimani hasa pale ambapo mgeni haelewi Kiswahili. Ukalimani hutumika pale ambapo mwanafunzi mgeni haelewi Kiingereza na husaidiwa na mwenzake ambaye anaelewa ama Kiswahili au Kiingereza. Pamoja na changamoto nyingi zinazojitokeza katika mbinu hii, bado lengo la ufundishaji hufikiwa na wageni wanaojifunza lugha hii hujifunza kwa urahisi na kwa furaha. Katika madarasa ya wageni, wanafunzi huuliza maswali mengine wakitaka wapewe tafsiri katika Kiswahili ya dhana fulani wanayoifahamu katika lugha zao. Kwa njia hii ufundishaji huwa rahisi na wenye mafanikio.

Tafsiri na Ukalimani katika Vyombo vya Habari vya Kiswahili na Mitandao

Katika masuala ya utangazaji, kwenye vyombo vya habari vinavyotumia Kiswahili, utangazaji umekuwa ukitumia tafsiri na ukalimani kama mbinu za kuwafikia watu wengi. Kwa mfano, kuna ukalimani wa alama katika Kiswahili kwenye vituo vya televisheni kama vile *TBC* na *ITV* na kuna ukalimani unaofanyika katika vituo vya redio kama vile *BBC Swahili*. Magazeti pia huchapisha taarifa mbalimbali ambazo zimepatikana kwa njia ya tafsiri. Tafsiri nyingi zinazofanyika nchini Tanzania ni kati ya Kiingereza na Kiswahili. Kwa ujumla, tafsiri na ukalimani ni taaluma zinazohitajika miongoni mwa waandishi wa habari na watangazaji.

Kwa upande mwingine, mitandao mbalimbali ya mawasiliano imekuwa ikitumia tafsiri ili kurahisisha mawasiliano miongoni mwa wanajamii. Mitandao ya simu imefanyiwa tafsiri katika Kiswahili na hivyo kuwarahisishia wazungumzaji wa lugha hizi kufanya uchaguzi wa lugha ambayo anaielewa vizuri. Huduma za kibenki za kimtandao pia zimefanyiwa tafsiri ili kurahisisha mawasiliano miongoni mwa watumiaji wa huduma hizi. Huduma nyingi za mtandaoni katika Kiswahili zina uteuzi wa ama lugha ya Kiingereza au Kiswahili. Mitandao ya mashirika ya umma na binafsi (hasa tovuti) imetengenezwa katika lugha mbili na kumpa mtumiaji uhuru wa kuchagua lugha anayoielewa zaidi.

Tafsiri ya Mashine na Ujanibishaji wa Programu za Kikompyuta

Hatua kubwa na ya kujivunia iliyofikiwa katika taaluma ya tafsiri na ukalimani katika Kiswahili ni ujanibishaji wa programu za *Microsoft* na *Open Source* (*Klinux*) katika Kiswahili. Pamoja na kwamba baadhi ya programu (kama vile *Microsoft*) zilikuwa zinaratibiwa nchini Kenya, shughuli kubwa au yote ya kutafsiri programu hizi ilifanyika nchini Tanzania, hasa kwa kushirikisha wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (TATAKI).

Tafsiri ya mashine pia imekuwa na mchango mkubwa katika tafsiri zinazofanyika nchini Tanzania. Watafitiwa wengi walioshiriki katika utafiti huu walieleza kwamba programu ya

Google (*Google Translate*) huwasaidia sana kutengeneza rasimu ya tafsiri. Pamoja na upungufu uliopo katika programu ya *Google*, programu hii imesaidia kukipa Kiswahili hadhi ya pekee, kama lugha ya kimtandao. Inawezekana kabisa *Google* hawakuwashirikisha wafasiri kutoka Tanzania lakini wamekuwa na mchango wao katika kuboresha tafsiri ya *Google* wanapoitumia.

Changamoto za Tafsiri na Ukalimani katika Kiswahili

Taaluma ya tafsiri na ukalimani hukabiliwa na changamoto mbalimbali. Kwa upande mwingine, kuna changamoto kadhaa zinazoikabili lugha ya Kiswahili kutokana na shughuli za ukalimani na tafsiri katika Kiswahili. Changamoto hizi zina athari kwa lugha na jamii kwa ujumla. Katika sehemu zinazofuata hapa chini tumejadili changamoto hizo kama zilivyoibuliwa na watu waliohojiwa katika utafiti huu.

Mfumuko wa Istilahi

Kuna mfumuko mkubwa wa istilahi na (au) msamiati ambao unakilemea Kiswahili. Msamiati huu unatokana na vitendo vya kila siku vya tafsiri na ukalimani. Katika shughuli hizi wakati mwingine wafasiri au wakalimani hukabiliwa na maneno, istilahi au dhana ambazo hazina visawe katika Kiswahili. Katika mazingira haya, istilahi au msamiati unaoundwa huingia moja kwa moja katika matumizi. Changamoto iliyopo ni kwamba maneno yanayoundwa hutumika bila kujali kama yamesanifishwa au la. Halikadhalika, wakati mwingine wafasiri tofauti huunda istilahi au msamiati tofauti kwa dhana moja. Hii inajidhihirisha katika maneno yanayotumika katika matumizi ya Kiswahili. Katika uwanja wa Kompyuta, kwa mfano, si ajabu kukutana na visawe vifuatavyo vikirejelea dhana moja:

Jedwali 3: Istilahi tofauti kwa dhana moja

	Istilahi ya Kiingereza	***Visawe vinavyotumika katika Kiswahili***
	Computer	Kompyuta, Ngamizi, Tarakilishi
	Population	Populesheni, wango, watafitiwa
	Cell phone	Simu seli, simu ya mkononi, selula, simu ya kiganjani, rununu
	Home page	Ukurasa masikani, Gombo kaya
	Search	Tafuta, Tafutiza au Sachi
	Methodology	methodolojia, mbinu za utafiti
	Printer	Kichapishi, Printa
	Masters Degree	Shahada ya Uzamili, Shahada ya Umahiri

Chanzo cha data: Malangwa (2008 & 2013)

Kama inavyoonekana hapo juu, kuna mkanganyiko mkubwa unaosababishwa na wafasiri kama matokeo ya kujiundia istilahi na kukosa ushirikiano wa karibu miongoni mwao. Ajabu ni kwamba hakuna juhudi zinazofanyika kushughulikia na kudhibiti maneno yanayozalishwa. Pengine suala la kujiuliza katika makala haya ni hili, nini kifanyike ili kudhibiti mwenendo huu? Yamkini, siyo rahisi kutoa pendekezo litakalokubalika na wengi. Suala la msingi hapa ni kwamba vyombo mbalimbali vya lugha ya Kiswahili katika ukanda wa Afrika Mashariki vinapaswa kuangalia namna nzuri ya kudhibiti mwenendo huu ili kuleta urari katika mawasiliano.

Malangwa (2010) aliangalia machafuko yanayosababishwa na wafasiri kwa kurejelea tafsiri ya programu za kompyuta iliyofanywa kwa ufadhili wa Microsoft (MS) na Klinux (KL). Tofauti ifuatayo ya kimsamiati/kiistilahi ilijitokeza:

Jedwali 4: Utofauti wa Istilahi/Maneno katika Tafsiri za MS na KL

Neno au Istilahi ya Lugha Chanzi	***Tafsiri ya MS***	***Tafsiri ya KL***
Password	Neno siri	Nywila
Computer	Ngamizi	Kompyuta
Internet	Tovuti	Intaneti *Mdahalishi[2]
Search and replace	Tafutiza na badilisha	Sachi na badilisha
Cache	Kirudufu data	Kache
Cursor	Kielekezi	Kasa
Full screen	-a kiwamba kizima	-a skrini nzima
Format	Umbizo	Fomati
Search engine	Mtambo tafutizi	Injini tafuti
File	Jalada	Faili

Chanzo cha data: Malangwa (2008)

Data hii inaonesha kwamba pamoja na kuwa wafasiri hawa walikuwa katika nchi moja (Tanzania) na wengi wao walitoka katika chuo kimoja, wafasiri hawa hawakuwa na mawasiliano wala majopo ya kujadili na kubadilishana istilahi. Kila mmoja alifanya shughuli hii kana kwamba hakuna mwingine anayeshughulika na hili. Hali hii pia inajidhihirisha katika mifano iliyotolewa katika jedwali lifuatalo:

Jedwali 5: Mifano zaidi kuhusu Utofauti wa Istilahi/Maneno katika Tafsiri za MS na KL

Neno au Istilahi ya Lugha Chanzi	***Tafsiri ya MS***	***Tafsiri ya KL***
Toolbar	Pauzana	Mwambaa zana
Bulleted list	Orodha aridhishe	Orodha tobwe
Webpage	Ukurasa Wavuti	Gombo Wavu
Website	Wavuti	Tovuti
Gateway	Kichanganishi Mtandao	Lango
Internet address	Anwani tovuti	Anwani wavuti
Install	Sanidi	Sakinisha
Keyboard	Kicharazio	Baobonye
Navigate	Abiri	Rambaza
Recycle bin	Kijalala	Kisuduru
Screensaver	Kinusuru kiwamba	Kilezi
Save	Akibisha	Hifadhi
Offline	Nje ya mtandao	Nje ya mkondo
Minimize	Punguza	Finya

Chanzo cha data: Malangwa (2008)

Katika kutazama data hii maswali ya kujiuliza ni: Je, hali hii inatupeleka wapi? Tunaweza kuzishawishi kweli nchi zione umuhimu wa kukikubali Kiswahili kitumike kama lugha rasmi au

[2] Hii ni kwa mujibu wa watafitiwa ambao ni wazungumzaji wa Kiswahili. Inatumika pia na wafasiri wengine wa mitandao ya kikompyuta katika Kiswahili.a

hata ya kufundishia? Hali hii kwa hakika inaashiria haja kubwa ya usanifishaji wa istilahi zinazoundwa kila uchao. Usanifishaji huu unapaswa kufanyika kikanda kwani tofauti ya istilahi au msamiati hasa katika maeneo ya kitaaluma ni ya kikanda zaidi (yaani, Ukanda wa Afrika Mashariki ambako Kiswahili kinatumika).

Mfumuko wa Wafasiri na Wakalimani Uchwara

Katika miaka ya karibuni wamejitokeza wafasiri na wakalimani wengi katika Kiswahili ambao hawana ujuzi wa taaluma hizi. Wafasiri hawa, kwanza hawana chombo kinachowaunganisha. Pili, hakuna makongamano yanayowaweka pamoja ili kuweza kujadiliana na kusaidiana katika kuimarisha shughuli za ukalimani. Hali hii inasababisha kujifanyia tafsiri au ukalimani kama wanavyopendelea. Tafsiri nyingi zinazotolewa ni mbovu na wakati mwingine haziwavutii wasomaji wake. Ajabu zaidi ni kwamba waliowapa shughuli hii huendelea kuzitumia kazi hizo na hata kuzichapisha. Hili nalo linahitaji kuwekewa mikakati ya kulishughulikia.

Uhaba wa Wataalamu

Uwepo wa wakalimani na wafasiri uchwara ni dalili kwamba taaluma hizi hazina wataalamu wa kutosha. Taaluma za tafsiri na ukalimani zimetambulishwa kwa kuchelewa sana katika taaluma za Kiswahili. Taasisi nyingi za elimu zimeanzisha taaluma hizi kwa kuchelewa sana ikilinganishwa na taaluma nyingine tumizi. Kwa mfano, nchini Tanzania taaluma ya tafsiri na ukalimani (katika Kiingereza na Kiswahili) imeanza kufundishwa katika miaka ya 1980. Hii ni sawa na kukumbuka shuka wakati kumekucha. Taaluma hii imeanzishwa katika kipindi ambapo vitendo vya tafsiri na ukalimani vimeshamiri. Hata hivyo, ikiwa vijana wetu wataandaliwa mapema na kuwasaidia kukuza na kuimarisha ujuzi wao katika taaluma hizi, bila shaka katika siku za usoni kutatokea wataalamu wa kuaminika.

Aidha, pamoja na jitihada za kufundisha tafsiri katika ngazi ya sekondari na vyuo, kuna tatizo kubwa la uhaba wa walimu wenye sifa. Takwimu zinaonyesha kwamba walimu wengi wanaofundisha tafsiri vyuoni ni wataalam wa masuala ya isimu tu ambao walisoma kozi ya tafsiri kama somo la hitiari. Viwango vya elimu vya waalimu hawa ni vya ama uzamili au shahada za awali (Tazama Jedwali 2 hapo juu). Walimu walio wengi wana kiwango cha elimu cha ngazi ya mahiri katika Kiswahili na wamesoma tafsiri kama sehemu ya kozi za isimu ya Kiswahili. Hii haiwafanyi wawe wabobevu katika tafsiri na ukalimani. Kama ilivyoelezwa hapo juu, walimu wengi wanaofundisha ukalimani hawajawahi kusoma kozi ya ukalimani na hivyo hufundisha kwa kutumia uzoefu wa taaluma ya tafsiri na kusoma machapisho yaliyopo ya taaluma ya ukalimani.

Nchini Tanzania tafsiri na ukalimani hufundishwa kama mada mojawapo kwenye masomo ya lugha (Kiswahili na Kiingereza) katika ngazi ya sekondari (yaani, kidato cha tano na sita). Katika shule za sekondari changamoto ni ile ile. Kuna uhaba mkubwa wa walimu wenye ujuzi na taaluma ya tafsiri na ukalimani. Kama ilivyoonekana hapo juu, taaluma hizi zimetambulishwa katika taaluma za Kiswahili kwa kuchelewa na hivyo walimu wengi wanaofundisha sekondari hawakupata fursa ya kusoma tafsiri na ukalimani katika mafunzo yao. Kwa mantiki hiyo, walimu wengi wanafundisha kwa kubabaisha kwani wanategemea kusoma vitabu vilivyopo tu. Hii ni hatari kubwa na haitusaidii kupata wataalamu wa tafsiri na ukalimani kwa mtindo huu. Mikakati inahitajika ili kuhakikisha kwamba walimu waliopo wanasaidiwa kupata mafunzo au semina za kuwasaidia kupata ujuzi wa taaluma hizi.

Uhaba wa Rasilimali na Vifaa

Pamoja na jitihada za kufundisha taaluma hii katika Idara za Kiswahili kwenye vyuo mbalimbali nchini Tanzania, na hata katika shule za sekondari, kuna uhaba mkubwa wa vitabu na makala zilizoandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Vitabu vingi vilivyopo na vinavyotumika kufundishia taaluma hii vimeandikwa katika lugha ya Kiingereza au Kifaransa, ambavyo pia ni vichache na upatikanaji wake ni mdogo. Wanafunzi na walimu hulazimika kuazima au kutoa nakala ya machapisho yaliyopo.

Aidha, kwa kipindi hiki chote na kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia ingetarajiwa kwamba mpaka sasa kungekuwa na nyenzo mbalimbali za kuwezesha ufundishaji wa tafsiri ya kikompyuta (tafsiri mashine). Pamoja na kuwa *Google* imeandaa programu ya tafsiri mashine, ni wachache sana wanaojua namna ya kuitumia na hata upatikanaji wake. Kuna baadhi ya mashirika kama vile ya kidini ambayo hufundisha wafasiri wao namna ya kutumia programu za kompyuta katika tafsiri zao (mfano, wafasiri wa *SIL International*). Hali hii inadokeza haja ya kuweka mikakati ya kuandaa programu za kutafsiri kwa kutumia mashine na kuanza kufundisha kipengele hiki katika kozi za tafsiri.

Mapendekezo na Hitimisho

Mapendekezo

Katika utafiti huu mapendekezo yafuatayo yamejitokeza:

i. Kuna haja kubwa ya kuwa na chombo (Chama) cha kuwaunganisha wafasiri na wakalimani nchini Tanzania na katika kanda ya Afrika mashariki.

ii. Kuna haja ya vyombo kama BAKITA kudhibiti na kusanifisha istilahi za Kiswahili. Vyombo hivi pia viwe vinatoa matamko mapema kabla maneno/istilahi hazijaenea sana na kuwa na mashiko.

iii. Juhudi za usanifishaji wa Kiafrika Mashariki zifufuliwe na kuratibiwa vizuri. Sasa kuna tume ya Kiswahili katika Afrika Mashariki. Tume hii iweke mikakati ya namna ya kusanifisha istilahi na msamiati wa Kiswahili katika ukanda huu.

iv. Kuwe na makongamano ya istilahi, tafsiri na ukalimani, ili kuwaunganisha wataalamu na kushirikisha ujuzi na uzoefu.

v. Pana haja ya kuweka mikakati ya kuandaa wataalamu wa tafsiri na ukalimani watakaotumika kufundisha na kufanya shughuli za ukalimani na tafsiri.

vi. Wataalamu wachache waliopo wasaidie kuandaa machapisho ya taaluma hizi katika Kiswahili ili kuwasaidia walimu na wanafunzi kufundisha kwa ufanisi badala ya kutegemea marejeleo ya Kiingereza.

vii. Kutokana na uhaba wa wataalamu na changamoto nyingine zinazohusiana na ufundishaji wa tafsiri na ukalimani katika vyuo vikuu nchini Tanzania, inapendekezwa hapa kwamba mamlaka za vyuo vikuu na idara zinazohusika ziandae na kufundisha taaluma hizi kama shahada inayojitegemea. Kutokana na umuhimu wake, ni vyema kuandaa wataalamu waliobobea katika uwanja huu kuanzisha shahada za awali.

Hitimisho

Katika mjadala huu imebainika kwamba pamoja na changamoto zilizopo katika taaluma ya tafsiri na ukalimani, taaluma hizi zina mchango mkubwa katika lugha ya Kiswahili na jamii kwa ujumla. Halikadhalika, kuna maendeleo makubwa yaliyofikiwa kuhusiana na taaluma hizi na

ambayo kama yatapewa uzito unaostahili, kuna ewezekano wa taaluma hizi kupanuka na kuwa na ubora unaokubalika katika viwango vya kimataifa. Wataalamu wachache wa tafsiri na ukalimani waliopo kwa kushirikiana na taasisi za lugha waandae mikakati kuboresha ufundishaji wa taaluma hizi na kuandaa wafasiri na wakalimani watakaofanya kazi hii kwa viwango vinavyokubalika. Utafiti huu umeonyesha kwamba kuna tatizo kubwa la kiistilahi linaloleta machafuko katika mawasiliano ya kitaaluma kwa kutumia Kiswahili. Istilahi zinaundwa kiholela na hivyo kusababisha kuwa na istilahi nyingi zinazorejelea dhana moja. Hali hii inahitaji mikakati ya usanifishaji ili kupunguza matatizo haya.

Marejeleo

Iida, A. (2008). Individual Differences in the Translation Process: Differences in the Act of Translation between two Groups of ESL Japanese Students. *Translation Journal*, www.translationdirectory.com, Accessed 12th April, 2011.

Ghadhi, A. S. (2010) Teaching Translation. *Translation Journal*, April 2010 www.translationdirectory.com, Accessed 12th September, 2011.

Malangwa, P.S. (2008) "Ukiushi katika Kutafsiri Matini za Kifasihi: Mifano kutoka Tafsiri ya Julius Kambarage Nyerere: *Mabepari wa Venisi*." Katika *Kiswahili*. Dar es Salaam, TUKI. Juz. 71, kur. 24-33.

Malangwa, P.S. (2012) "Overcoming the barriers through literal and descriptive translations: Examples of Kanga names" katika *Journal for Studies in Humanities and Social Sciences*, Juz. 1, Na. 1, 51-62.

Mwansoko, H. J. M., na Wenzake (2006) *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu*. Dar es Salaam: TUKI.

Mshindo, H. (2010) *Tafsiri na Kufasiri*. OUP: Dar es Salaam.

Taasisi ya Elimu Tanzania (1996) *Kiswahili Kidato cha Kwanza*. Dar es Salaam: TIE.

Taasisi ya Elimu Tanzania (1996) *English for Sekondary Schools Book One.* Dar es Salaam: TIE.

Wanjala, F. S. (2011). *Misingi ya Ukalimani na Tafsiri*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers.